

KUMB: PPR/17 - 09/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 6 SEPTEMBER 2017**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Septemba 2017**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Agosti 2017. Kwa mwezi Septemba 2017, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 10/lita (sawa na asilimia 0.53) na Shilingi 57/lita (sawa na asilimia 3.10) sawia, wakati bei ya Mafuta ya Taa imepungua kwa Shilingi 19/lita (sawa na asilimia 1.04). Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli nazo zimeongezeka kwa Shilingi 10.41/lita (sawa na asilimia 0.56) na Shilingi 56.74/lita (sawa na asilimia 3.30) sawia, wakati bei ya jumla ya Mafuta ya Taa imepungua kwa Shilingi 19.01/lita (sawa na asilimia 1.11). Ongezeko la bei za Petroli na Dizeli kwenye soko la ndani, limetokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia na ongezeko la gharama za usafirishaji wa mafuta hayo (*BPS premiums*). Kupungua kwa bei ya Mafuta ya Taa kunatokana na kupungua kwa gharama za usafirishaji wa mafuta hayo (*BPS premiums*) ijapokuwa bei ya mafuta hayo imeongezeka katika soko la dunia.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote katika mkoa wa Tanga nazo zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Agosti 2017. Kwa mwezi Septemba 2017, bei za rejareja za Petroli zimeshuka kwa Shilingi 13/lita (sawa na asilimia 0.65) wakati bei za Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 14/lita (sawa na asilimia 0.78) na Shilingi 106/lita (sawa na asilimia 6.21) sawia. Aidha, bei za jumla za Petroli zimeshuka kwa Shilingi 12.98/lita (sawa na asilimia 0.69) wakati bei za Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 14.47/lita (sawa na asilimia 0.83) na Shilingi 105.88/lita (sawa na asilimia 6.65), sawia. Kupanda na kushuka kwa bei za mafuta mkoani Tanga kunatokana na mabadiliko ya bei za mafuta hayo katika soko la dunia na ongezeko la gharama za usafirishaji wa mafuta hayo (*BPS premiums*). Sambamba na maelezo haya, ni vizuri ifahamike ya kwamba, katika mkoa wa Tanga, mzigo mpya wa Mafuta ya Taa ulipokelewa mwezi Septemba 2016, wakati mzigo mpya wa Petroli na Dizeli ulipokelewa mwezi Juni 2017.
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma ya kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (e) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017.****
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (g) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti cha wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shilingi/Lita)	Dizeli (Shilingi/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shilingi/Lita)
Dar es Salaam	1,989	1,887	1,811
Arusha	2,073	1,971	1,895
Arumeru (Usa West)	2,073	1,971	1,895
Karatu	2,091	1,989	1,913
Monduli	2,078	1,976	1,900
Monduli-Makuyuni	2,083	1,981	1,905
Ngorongoro (Loliondo)	2,164	2,062	1,986
Kibaha	1,993	1,891	1,815
Bagamoyo	2,000	1,898	1,822
Kisarawe	1,996	1,894	1,818
Mkuranga	1,999	1,897	1,821
Rufiji	2,016	1,914	1,838
Dodoma	2,048	1,945	1,870
Bahi	2,055	1,953	1,877
Chemba	2,074	1,972	1,896
Kondo	2,080	1,978	1,902
Kongwa	2,045	1,943	1,867
Mpwapa	2,049	1,947	1,871
Iringa	2,053	1,951	1,875

Kilolo	2,057	1,955	1,879
Mufindi (Mafinga)	2,063	1,961	1,885
Njombe	2,081	1,979	1,903
Ludewa	2,119	2,017	1,941
Makete	2,112	2,010	1,934
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,079	1,977	1,901
Bukoba	2,204	2,102	2,026
Biharamulo	2,178	2,076	2,000
Karagwe (Kayanga)	2,220	2,118	2,042
Kyerwa (Ruberwa)	2,226	2,124	2,048
Muleba	2,204	2,102	2,026
Ngara	2,169	2,067	1,991
Misenyi	2,212	2,110	2,034
Geita	2,154	2,052	1,976
Bukombe	2,143	2,041	1,965
Chato	2,175	2,073	1,997
Mbogwe	2,192	2,090	2,014
Nyang'hwale	2,169	2,067	1,991
Kigoma	2,220	2,118	2,042
Uvinza (Lugufu)	2,232	2,130	2,054
Buhigwe	2,209	2,107	2,031
Kakonko	2,177	2,075	1,999
Kasulu	2,206	2,104	2,028
Kibondo	2,184	2,082	2,006
Moshi	2,062	1,960	1,884
Hai (Bomang'ombe)	2,066	1,964	1,888
Mwanga	2,056	1,954	1,878
Rombo (Mkuu)	2,083	1,981	1,905
Same	2,049	1,947	1,871
Siha (Sanya Juu)	2,069	1,967	1,891
Lindi	2,048	1,946	1,870
Lindi-Mtama	2,066	1,964	1,888
Kilwa Masoko	2,023	1,921	1,845
Liwale	2,069	1,966	1,891
Nachingwea	2,077	1,975	1,899
Ruangwa	2,078	1,976	1,900
Babati	2,111	2,009	1,933
Hanang (Katesh)	2,121	2,019	1,944
Kiteto (Kibaya)	2,122	2,020	1,944
Mbulu	2,124	2,022	1,946
Simanjiro (Orkasumet)	2,143	2,041	1,965
Musoma	2,167	2,065	1,989
Musoma Vijijini (Busekela)	2,208	2,106	2,030
Rorya (Ingirijuu)	2,176	2,074	1,998
Rorya (Shirati)	2,211	2,109	2,033

Bunda	2,158	2,056	1,980
Butiama	2,164	2,062	1,986
Serengeti (Mugumu)	2,213	2,110	2,035
Tarime	2,178	2,076	2,000
Mbeya	2,096	1,994	1,918
Chunya	2,105	2,003	1,927
Chunya (Makongolosi)	2,119	2,017	1,941
Ileje	2,109	2,007	1,931
Kyela	2,111	2,009	1,934
Mbarali (Rujewa)	2,080	1,978	1,902
Mbozi (Vwawa)	2,105	2,003	1,927
Momba (Chitete)	2,114	2,012	1,936
Rungwe (Tukuyu)	2,105	2,003	1,927
Morogoro	2,014	1,912	1,836
Mikumi	2,029	1,927	1,851
Kilombero (Ifakara)	2,052	1,950	1,874
Kilombero (Mlimba)	2,074	1,972	1,896
Kilombero (Mngeta)	2,063	1,961	1,885
Ulanga (Mahenge)	2,062	1,960	1,884
Malinyi	2,072	1,970	1,894
Kilosa	2,032	1,930	1,854
Gairo	2,032	1,930	1,854
Mvomero (Wami Sokoine)	2,024	1,922	1,846
Turian	2,039	1,937	1,861
Mtwara	2,061	1,959	1,883
Nanyumbu (Mangaka)	2,110	2,008	1,932
Masasi	2,087	1,985	1,909
Newala	2,093	1,991	1,915
Tandahimba	2,086	1,984	1,908
Mwanza	2,139	2,037	1,961
Kwimba	2,175	2,073	1,997
Magu	2,147	2,045	1,969
Misungwi	2,144	2,042	1,966
Sengerema	2,171	2,069	1,993
Ukerewe	2,198	2,096	2,020
Sumbawanga	2,161	2,059	1,983
Kalambo (Matai)	2,154	2,052	1,976
Nkasi (Namanye)	2,175	2,073	1,997
Katavi (Mpanda)	2,196	2,094	2,018
Mlele (Inyonga)	2,175	2,073	1,997
Songea	2,112	2,010	1,934
Mbinga	2,145	2,043	1,968
Namtumbo	2,141	2,039	1,963
Nyasa (Mbamba Bay)	2,148	2,046	1,970
Tunduru	2,171	2,069	1,993

Shinyanga	2,117	2,015	1,939
Kahama	2,131	2,029	1,953
Kishapu	2,146	2,044	1,968
Simiyu (Bariadi)	2,159	2,057	1,981
Busega (Nyashimo)	2,152	2,050	1,974
Itilima (Lagangabilili)	2,162	2,060	1,984
Maswa	2,150	2,048	1,972
Meatu (Mwanhuzi)	2,157	2,055	1,979
Singida	2,079	1,977	1,901
Iramba	2,091	1,989	1,913
Manyoni	2,064	1,962	1,886
Ikungi	2,075	1,973	1,897
Mkalama (Nduguti)	2,104	2,002	1,926
Tabora	2,143	2,041	1,965
Igunga	2,097	1,995	1,919
Kaliua	2,161	2,059	1,983
Ulyankulu	2,155	2,053	1,977
Nzega	2,107	2,005	1,929
Sikonge	2,154	2,052	1,977
Urambo	2,156	2,054	1,978
Tanga	1,993	1,877	1,810
Handeni	2,013	1,897	1,830
Kilindi	2,028	1,912	1,845
Korogwe	2,005	1,889	1,822
Lushoto	2,014	1,898	1,831
Mkinga (Maramba)	2,000	1,884	1,817
Muheza	1,998	1,881	1,814
Pangani	1,999	1,883	1,816

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	1,877.88	1,775.85	1,699.92

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	1,881.70	1,765.56	1,698.68

Mhandisi Godwin Samwel
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA